



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI  
(Barua zote zijibiwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)**



**S. L. P. 109,  
BARIADI.**

**Kumb.Na.BC.22/124/04A/97**

**Tarehe 25/08/2023**

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi amepokea kibali cha ajira mpya chenye Kumb.Na FA.170/533/01"B"/103 cha tarehe 04/7/2023 kibali cha ajira chenye kumb Na FA.170/533/01"B"/97 cha tarehe 23 Mei 2023 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hivyo,anakaribisha kutuma maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi kama ilivyoainishwa katika tangazo.

**MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III (NAFASI 07)**

**1.1 Sifa za mwombaji**

Awe amehitimu elimu ya kidato cha nne au sita na ambaye amehitimu Astashahada/cheti (NTA level 5) katika mojawapo ya fani zifuatazo; utawala, usimamizi wa rasilimali watu, sheria, mipango ya maendeleo vijijini, elimu ya jamii na usimamizi wa fedha kutoka vyuo vinavyotambuliwa na serikali.

**1.2. Mshahara**

Cheo cha Mtendaji wa Kijiji daraja la III kina mshahara wa TGS B/I

**1.3 Kazi na Majukumu ya Mtendaji wa Kijiji daraja la III**

- Afisa Masuuli na mtendaji mkuu wa serikali ya kijiji.
- Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na Msimamizi wa Utawala Bora.
- Kusimamia na kuratibu upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijijini.
- Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali.



- Kutafsiri na kusimamia Sera ,Sheria na taratibu za Serikali
- Kiongozi wa wakuu wa vitengo na kitaaluma katika kijiji.
- Mratibu wa utekelezaji wa sera sheria zinazotekelezwa na Halmashauri katika kijiji.
- Mshauri wa kamati ya Kijiji kuhusu mipango ya maendeleo katika Kijiji
- Msimamizi wa utekelezaji wa sheria ndogo pamoja na sheria nyingine zinazotumika katika kijiji.
- Mshauri wa kamati ya Kijiji kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama.
- Msimamizi wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umasikini katika kijiji.
- Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote.
- Kuandaa na kutunza rejesta ya wakazi wote wa kijiji, na
- Atawajibika kwa Mtendaji wake wa Kata.

#### 4.0 Masharti ya Ujumla.

- Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- Barua za maombi ziandikwe kwa Mkono na kutumwa kwa anuani iliyotajwa hapo chini.
- Mwombaji aambatanishe nakala za vyeti vya taaluma,vyeti vya Elimu na cheti cha kuzaliwa.Mwombaji atakayewasilisha “result slip” statement of result” au provisional of result maombi yake **hayatakubaliwa**, Aidha mwombaji awe na cheti chenye NTA level 5.
- Mwombaji awasilishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu.(Referees) wakuaminika
- Watakao itwa kwenye usaili (Interview) ni wale tu watakaokidhi vigezo na masharti yaliyotolewa hapo juu.


Mwisho wa kupokea maombi itakuwa tarehe **08/09/2023 saa 9:30 Alasiri.**

Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo;-

**MkurugenziMtendaji  
Halmashauri ya Wilaya  
S.L.P 109  
BARIADI**

Tangazo hili linapatikana katika tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi [www.bariadidc.go.tz](http://www.bariadidc.go.tz) , mbao za Matangazo na kwenye “website” ya Sekretarieti ya ajira.

IMETOLEWA NA

  
STEPHEN T. MASUNGWA  
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
BARIADI

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA BARIADI**